
# Ukuaji wa Uchumi Tanzania: Je, Unapunguza Umaskini?

**Dondoo za Sera 1.09**




## Utangulizi

Tanzania imesifiwa sana kuwa inaendesha uchumi wake katika njia sahihi. Katika chapisho la hivi karibuni, **"Tanzania: the story of an African transition",** shirika la fedha duniani IMF, linadai kuwa katika miongo miwili iliyopita, uchumi wa Tanzania umepitia kipindi cha mpito chenye mafanikio, ambapo uchumi huria na mageuzi ya kitaasisi yamepelekea kuongezeka kwa pato la taifa hadi kufikia zaidi ya 7% kwa mwaka tangu 2000.

Je, katika ukuaji huu wa uchumi umefanikisha kuboresha maisha ya Watanzania? Angalizo hili linaonesha kuwa kipindi hiki cha "mpito wenye mafanikio" yametokea yafuatayo:

- Umaskini umeshindwa kupunguzwa
- Mafanikio mengi yanaonekana Dar es Salaam na siyo vijijini, na
- Maskini wanaendelea kuwa maskini zaidi na matajiri kutajirika zaidi

Wakati huo huo

- Tanzania inabaki nyuma katika kufanikisha malengo ya milenia katika shabaha ya kupunguza umaskini na kutekeleza MKUKUTA, na
- Tanzania inaelekea kubaya zaidi ukilinganisha na nchi zinginezo barani Afrika na Asia

## Ukweli 1: Kipindi cha mpito cha uchumi hakijapunguza umaskini inavyostahiki

Tafiti zilizofanywa na Taasisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) zinaonesha kutokuwapo kwa dalili zozote za kupunguza umaskini. Kati ya mwaka 2001 na 2007 sehemu ndogo sana ya Watanzania maskini walipunguza umasikini (NBS 2001; 2007). Kupungua huko ni kudogo mno kiasi ambacho si rahisi kujigamba kwa uhakika kama umaskini ulishuka, au kama ulibaki vivyo hivyo.

**Jedwali 1: Matokeo ya umaskini tangu 1991**

| | 1991 | 2001 | 2007 |
|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 28.1 | 17.6 | 16.0 |
| Miji mingine | 28.7 | 25.8 | 24.2 |
| Vijijini | 40.8 | 38.6 | 37.4 |
| Tanzania Bara | 38.6 | 35.6 | 33.4 |

*Chanzo: National Bureau of Statistics 2001 & 2007*

Kwa ujumla, katika kipindi cha miaka 16 kati ya 1991 na 2007, umaskini ulipungua kwa 5%. Lakini sehemu kubwa ya mabadiliko haya yanaashiria kutokea Dar es Salaam. Maeneo ya vijijini, na maeneo mengine ya mijini, kupungua kwa umaskini ni kudogo mno ambako hakutupi imani kwamba kwa hakika umaskini umepungua.

## Ukweli 2: Kuna maskini wengi zaidi leo kuliko 2001

Wakati ambapo asilimia ya watu wanaoishi katika umaskini (yaani chini ya shilingi 500 kwa mtu kwa siku, angalia kisanduku 1) ulishuka kidogo tangu 2000/1, kwa kuwa idadi ya watu imeongezeka, katika kipindi hicho hicho, jumla ya watu wanaoishi chini ya kiwango cha chini cha umaskini iliongezeka hadi kufikia million 1.3 (Angalia Jedwali 2 hapa chini).

**Jedwali 2: Kuongezeka kwa idadi ya maskini (katika mamilioni) kati ya 2001 na 2007**

| | Idadi ya watu (TZ Bara mil.) | Kiwango cha Umaskini (%) | Idadi ya watu maskini (mil.) |
|---|---|---|---|
| 2001 | 32.4 | 35.6 | 11.5 |
| 2007 | 38.3 | 33.4 | 12.8 |

**Ongezeko la idadi ya maskini: milioni 1.3**

*Chanzo: Economic Survey – Jedwali 33, National Bureau of Statistics 2001 & 2007*

**Kisanduku 1: Tunapimaje umaskini?**


Kwa Tanzania, watu hufikiriwa kuwa ni maskini pale ambapo ulaji wao uko chini ya kiwango cha taifa cha umaskini, ambapo ulaji hujumuisha vitu vyote vinavyonunuliwa na vinavyozalishwa na kuliwa nyumbani, kama vile chakula, vifaa vya nyumbani, nguo, mali binafsi, huduma binafsi, starehe, usafi, huduma za nyumbani, michango, nishati, sabuni na sigara. Si kila vitu vinavyoliwa au kutumika vinajumuishwa katika kukadiria umaskini. Mathalani, gharama za afya, elimu na maji havijumuishwi.

Kiwango cha chini cha Taifa cha umaskini kilikadiriwa na NBS mwaka 2001 kwa kuzingatia Utafiti wa Bajeti ya Kaya ya mwaka 2000/01. Huwakilisha gharama za vitu (chakula na bidhaa zingine) ambavyo kwa kawaida huliwa na kaya maskini. Mwaka 2001 kiwango cha chini cha taifa cha umaskini kilikuwa shilingi 7,253 kwa mtu kwa siku 28. Kwa kuongezeka bei ya vitu kwa 93% kati ya 2000/1 na 2007, kiwango cha chini cha umaskini 2007 ni Tshs 13,998 (7,253 x 1.93) au kwa wastani shilingi 500 kwa mtu kwa siku.

## Ukweli 3: Tangu 2001 matajiri walitajirika zaidi na maskini wakawa fukara zaidi

Si tu kwamba umaskini haukubadilika tangu 2000/1, kwa kuwa kaya fukara zaidi ziliendelea kuwa maskini zaidi, wakati ambapo kaya tajiri ziliendelea kutajirika zaidi kati ya 2000/1 na 2007. Hali hii inabainishwa kwenye mchoro hapa chini inayoonesha kiwango cha ukuaji wa ulaji kwa kila kundi la kipato. Kwa mhimili uliolala idadi ya watu imewekwa kutoka maskini zaidi kwenda matajiri zaidi, pakiwa na maskini upande wa kushoto wa mhimili na matajiri upande wa kulia.

### Mchoro 1: Mabadiliko ya ulaji tangu 2000/1 kulingana na kundi la kipato




*Chanzo: Development Partner Group, 2008*

Mchoro umekaa juu kabisa ya mstari wa sifuri, ikionesha kuwa karibu makundi yote ya kipato yaliongeza ulaji. Hata hivyo, ongezeko ni dogo, kwa wastani wa asilimia 0.8 kwa


mwaka, au asilimia 5 kwa kipindi kizima. Mchoro pia unaonesha kuwa asilimia 10 ya watu maskini kupindukia wana hali mbaya sana, yaani viwango vya ulaji wao vilishuka. Kwa ulinganifu, kaya tajiri zikawa na maisha bora. Hii inaonesha mwenendo unaotia hofu ambapo maskini wanabaki nyuma na matajiri kuendelea kutajirika.

## Ukweli 4: Tanzania haiku katika njia sahihi kutimiza shabaha ya MMM (MDG)/MKUKUTA

Tanzania imeridhia Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MMM - MDGs). Lengo la kwanza linaitaka Tanzania kupunguza umaskini kati ya 1990 na 2015 kwa 50%. Mwaka 1991/92 umaskini Tanzania ulikuwa 38%, hivyo lengo ni kupunguza umaskini hadi 19% ifikapo 2015. Mchoro namba 2 hapa chini unabainisha kuwa Tanzania iko nje katika kufikia shabaha hii. Mihimili katika mchoro inaonesha viwango halisi vya umaskini, na mstari mwembamba unaonesha mwenendo uliopo, ambapo mstari mnene unaonesha kupungua kwa umaskini, mahali ambapo Tanzania inapaswa kutimiza ili kufikia lengo la Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MMM – MDG).

Ni wazi kuwa tayari kunako mwaka 2000/01 Tanzania ilikuwa nje ya njia sahihi kwa kuwa mhimili ulizidi mstari wa mwenendo kwa 5.9%. Kati ya 2001 na 2007 hali ikazidi kuwa mbaya zaidi kwa kuwa mhimili sasa unazidi mstari wa mwenendo kwa wastani wa 7.6%. Kwahiyo shabaha ya MKUKUTA, ambayo inalenga kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MMM) ifikapo 2010, iko nje kabisa ya matarajio.

### Mchoro 2: Matokeo ya umaskini kulingana na mstari wa mwenendo wa MMM (MDG)





*Chanzo: Development Partner Group, 2008*

## Ukweli 5: Tanzania imefanya vibaya ukilinganisha na nchi zingine

Ufanisi wa Tanzania katika kupunguza umaskini uko vibaya ukilinganisha na nchi za kiwango chake, ambazo kama Tanzania zilikuwazinatekeleza vizuri uchumi (sera) na ambazo pia zilifanya mageuzi ya kiuchumi kwenye ukanda wao katika Afrika (Ghana, Uganda) na Asia (Vietnam na India). Wakati Tanzania idadi ya watu maskini ilipungua kwa 2.4% kati ya 1991 na 2007, kwa Uganda, Ghana na Vietnam ilipungua karibu mara 10 zaidi: kwa wastani wa 23% hadi 24%. India nayo ilifanikiwa kupunguza idadi hiyo kwa kikubwa (kwa 7%) kwa kipindi kifupi mno.

**Mchoro 3: Mabadiliko ya idadi ya watu maskini katika baadhi ya nchi**





*Chanzo: Development Partner Group, 2008*

## Ukweli 6: Takribani nusu ya watu hawana lishe bora

Lengo la kwanza la Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MMM) pia linalenga kupunguza baa la njaa. Tanzania imepiga hatua katika eneo hili na sehemu ndogo ya watoto wenye utapiamlo imepungua tangu 1991. Hata hivyo, watoto 4 kati ya 10 wenye miezi 0 hadi 59 wanakosa lishe bora, na takribani mtoto 1 kati ya kila 5 ana uzito mdogo sana.

Tukizingatia kuongezeka kidogo katika ulaji, kwa mwili kupata kalori kumeongezeka tangu 2001, ingawa kwa sehemu ndogo. Kama ambavyo mchoro namba 4 unavyobainisha hapa chini, takribani 25% ya watu hupata kalori mwilini kidogo sana za kuwezesha kuimarisha miili yao na kufanya kazi nyepesi za ofisini. Ni nusu tu ya watu ndio hupata kalori za kutosha mahitaji ya kufanya kazi nzito (kama kilimo). Pamoja na hayo, ni wale wanaopata kalori kidogo sana mwilini ndio wanaojihusisha na kazi nzito na ngumu.

**Mchoro 4: Upataji kalori mwilini kwa mtu mzima**




*Chanzo: Research & Analysis Working Group February 2009 (draft)*

Kwa kuongezea, Watanzania wanaendelea kuwa na lishe ya aina moja. Hali hii huongezea magonjwa yanayohusiana na viini lishe kama vile ukosefu wa madini ya joto (aidini), chuma na vitamini A. Kusema ukweli, hali hii hupelekea kupungua kwa nguvu kazi yenye tija na kuongezeka kuambukizwa maradhi. Utapiamlo huchangia 56% ya vifo vya utotoni Tanzania na ukosefu wa akili kwa 13%. Utafiti kutoka mkoani Kagera ulibaini kuwa watoto waliokosa lishe bora hupoteza hadi miaka 2 ya elimu ukilinganisha na wenzao wenye lishe bora (World Bank, 2007).

## Ukweli 7: Watu humiliki bidhaa zaidi, lakini thamani yake kiujumla hubakia ile ile


Tangu 2001 umilikaji wa bidhaa za kudumu kwa walaji uliongezeka vizuri. Umilikaji wa luninga uliongezeka zaidi ya mara tatu wakati ambapo umilikaji wa vyandarua uliongezeka maradufu. Bidhaa kama redio na baiskeli navyo viliongezeka vizuri, na umilikaji wa simu za mkononi ulishamiri: mwaka 2007 robo ya kaya zote zilimiliki angalau simu moja ya mkononi. Kuongezeka kwa ulaji wa bidhaa za kudumu unaangaliwa na kuboreka kwa hali ya makazi, japo kuna mabadiliko yasiyoridhisha (NBS 2008).

Kuongezeka katika umilikaji wa bidhaa za kudumu kunaashiria kuongezeka ustawi na pengine kwa namna fulani kunashangaza kwa kulinganisha na ongezeko dogo katika ulaji. Mabadiliko katika bei yanaonekana yako nje ya ongezeko hili. Kilichotokea ni

kwamba kaya zilianza kumiliki vitu vingi vya kudumu ambavyo vilianza kuwa nafuu na vitu vichache vilibakia ghali. Hili linajionesha kwenye mchoro namba 5 hapa chini. Bidhaa zilizoonekana kuongezeka zaidi, kama vile saa na vyandarua, ndizo ambazo bei zake zilishuka sana. Kinyume chake kilitokea kwa bidhaa ambazo zilikuwa ghali.

Kwa kuendana na mabadiliko kidogo katika ulaji, thamani ya bidhaa zilizomilikiwa kiujumla zilibakia vile vile. Tukiweka kando simu za mkononi, thamani ya bidhaa ilishuka kidogo. Tukijumuisha na simu za mkononi, thamani ya bidhaa kiujumla iliongezeka kwa 3% kama inavyojieleza kwenye bei za 2000/01.

## Figure 5: Changes in real prices and changes in ownership of consumer durables




*Chanzo: Poverty Monitoring Group, Rapid Poverty Assessment 2008 Angalizo: kupata badiliko halisi katika bei, kielelezo cha bei cha Fisher kwa ajili ya bidhaa (101%) hutolewa kutoka kwenye badiliko dogo la bei*

## Hitimisho

Uchumi wa soko huria Tanzania, kwa sasa umeshindwa katika jambo muhimu: kupunguza umaskini wa kipato kwa Watanzania wengi. Hii haimaanishi kukataa mafanikio katika nyanja zingine, (mathalani, watoto maskini hujiunga shule; na bidhaa nyingi humilikiwa), lakini inaonesha kuwa kwa Watanzania wengi  uwezo wa kujikimu wao wenyewe haujabadilika. Kwa taswira hii, ni vigumu kutetea kuwa kipindi cha mpito wa uchumi Tanzania kimeleta mafanikio. Kwa kuelezea changamoto hii kiukweli na tafakuri, kunahitajika kutoa kipaumbele cha juu katika ajenda za kisiasa na kisera.

Dondoo hii imetolewa na Policy Forum, kwa kushirikiana na Twaweza.

policy forum

**Policy Forum**
**S.L.P 38486-Dar es Salaam – Tanzania**
**Simu (225 22) 2772611, +255 782317434, Faksi: (255 22) 2772611**
**Barua pepe :info@policyforum.or.tz**
**Tovuti :-www.policyforum-tz.org**